Hayya'alla khayril A'mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:17 PM Page A

# HAYYA 'ALAA KHAYRI 'L-'AMAL KATIKA ADHANA

Kimeandikwa na:
**Sheikh Abdul Amir Sultan.**

Kimetarjumiwa na:
**Amiri Mussa Kea.**

Hayya'alla khayril A'mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:17 PM Page B

# ترجمة

## في رحاب أهل البيت عليهم السلام

جزئيّة

# حيّ على خير العمل

في الأذان

تأليف

الشيخ عبد الأمير السلطاني – لجنة البحوث

من اللغة العربية إلى اللغة السواحلية

Hayya'alla khayril A'mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:17 PM Page C

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**

**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN: 978 - 9987 - 512 - 58 - 4**

Kimeandikwa na:
**Sheikh Abdul Amiri Sultan.**

Kimetarjumiwa na:
**Amiri Mussa Kea.**

Kimepangwa katika Kompyuta na:
**Hajat Pili Rajab**

**Toleo la kwanza: Oktoba, 2011**
**Nakala: 1000**

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**

**Alitrah Foundation**

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: www.ibn-tv.com

Katika mtandao: www.alitrah.info

# Yaliyomo

Ibara: "Hayya' ala Khayrili A'mal katika Adhana............................2

Namna ilivyoanza adhana kwa Mujibu wa Ahlul Sunna...................3

Aliyoyapokea Imam Ahmad katika Musnad yake...........................15

Aliyoyapokea Imam Darmi katika Musnad yake............................16

Aliyoyapokea na Imam Malik katika kitabu chake Muwatwai........17

Yaliyopokewa na Ibn Sa'ad katika kitabu Wabaqaat......................18

Yaliyopokewa na Bayhaqi katika kitabu chake Sunan.....................20

Yaliyopokewa na Darul Qutni........................................................21

Namna ilivyoanza adhana kwa mujibu wa Ahlul bayt (a.s)............22

Maoni ya wanavyuoni kuhusu ibara "Hayya" Ala Khayril A'mali'.32

Nyongeza katika kutilia mkazo maelezo yahusuyo ibara "Hayya" Ala Khayril A'mali"...........................................................................40

Hayya'alla khayril A'mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:17 PM Page E



بسم الله الرحمن الرحيم

# Neno la Mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kwa jina la: "*Hayya'alla khayril A'Mali"*

Kitabu hiki kimeshughulikia tamko hili la Adhana ambalo limo katika Adhana ya Mashia na ambalo halimo katika Adhana ya Masunni.

Wanachouni wa Kiislamu kama kawaida ya wanadamu wamehitilafiana katika hukumu ndogo ndogo katika matendo ya ibada, lakini kama ilivyo, tofauti ndogo kati ya wanachuo kwa wafuasi inakuwa ni mlima wa tofauti na kusababisha zongo lisilo na maana. Mambo ambayo wanachuo wetu wamehitilafiana si katika asili au misingi ya dini, na isitoshe ni mambo machache sana ukilinganisha na yale tunayokubaliana nayo.

Kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya 'Al-Itrah Foundation' imeona ikitoe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili, kwa madhumuni yake yale yale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya dini na ya kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu, Hemedi Lubumba Selemani (Lipumba) kwa kukubali jukumu hili la kukifanyia tarjuma kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

**Mchapishaji:**
**Al-Itrah Foundation**
**S. L. P. 19701**
**Dar-es-Salaam, Tanzania.**

Hayya’alla khayril A’mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:17 PM Page F



# AHLUL BAYT KATIKA QUR’ANI TUKUFU

**Mwenyezi Mungu anasema:**

﴿ إِنَّمَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيُذۡهِبَ عَنكُمُ ٱلرِّجۡسَ أَهۡلَ ٱلۡبَيۡتِ وَيُطَهِّرَكُمۡ تَطۡهِيرٗا ﴿٣٣﴾ ﴾

**“Hakika Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu watu wa nyumba ya Mtume na anataka kukutakaseni sana sana”. (33:33)**

## AHLUL BAYT KATIKA HADITHI

Mtume (s.a.w.w) amesema: “Hakika mimi nawaachieni vizito viwili, kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu, ndugu zangu wa karibu; iwapo mtashikamana navyo hamtapotea kamwe baada yangu.”[1]

[1] Rejea: *Sahih* zote na *Musnad* zote.

# NENO LA JUMUIYA

Hakika mirathi ya Ahlul-Bait ambayo imehifadhiwa na kambi yao na wafuasi wao dhidi ya upotovu inaonyesha kambi iliyokusanya aina mbalimbali za taaluma za kiislamu.

Kambi hii imeweza kulea nafsi mbalimbali zilizo tayari kunywa kutoka kwenye chemchemu hiyo, na kuupa umma wa kiislamu wanavyuoni wakubwa wenye kufuata nyayo za ujumbe wa Ahlul-Bait.

Wanavyuoni waliokusanya vidodosa na maswali mbalimbali ya madhehebu na mitazamo tofauti ya kifikira kuanzia ndani ya desturi ya kiisilamu hadi nje ya desturi hiyo, huku wao wakitoa majibu na utatuzi makini juu ya maswali hayo ndani ya karne zote.

Jumuiya ya kimataifa ya Ahlul-Bait imefanya hima kutetea tukufu za ujumbe wa Uislamu na ukweli wake ambao umechafuliwa na makundi, madhehebu na wanaharakati mbalimbali wenye chuki na Uislamu.

Jumuiya imefuata nyayo za Ahlul-Bait na za wafuasi wa kambi yao njema ambayo imefanya hima kujibu madai yenye kuendelea na daima ikajaribu kubaki ndani ya msitari wa mapambano kwa kiwango kinachohitajika ndani ya kila zama.

Hakika uzoefu ambao umehifadhiwa ndani ya vitabu vya wanavyuoni wa kambi ya Ahlul-Bait katika dhamira hii ni wa aina ya pekee, kwa sababu una akiba ya kielimu inayotegemea akili na hoja, huku ukijiepusha na matamanio na upendeleo uliokatazwa.

Unazungumza na wasomi na wanafikra wenye fani maalumu, mazungumzo ambayo yanakubalika kiakili na yanapokewa na maumbile yaliyo salama.


Jaribio hili la Jumuiya ya kimataifa ya Ahlul-Bait limekuja kuwapa watafuta ukweli hatua mpya ya uzoefu wa thamani katika ulingo wa mazungumzo na maswali na kujibu hoja za utata zilizotolewa zama zilizopita au zinazotolewa leo kwa njia ya Tovuti, na hasa kwa kupewa nguvu na baadhi ya duru zenye chuki dhidi ya Uislamu na Waislamu.

Ikijiepusha na uchochezi uliokatazwa, na ni yenye kuhangaikia kuzishauri akili zenye kufikiria na nafsi zenye kutafuta haki, ili ziweze kufikia kwenye haki ambayo inatolewa na Kambi ya Ahlul-Bayt ulimwengu mzima, ndani ya zama ambazo akili inaerevuka na nafsi na roho zinaboreka kwa kasi ya pekee.

Ni lazima tugusie kuwa mfululizo huu wa tafiti hizi umeandaliwa na Kamati maalumu toka jopo la wanavyuoni watukufu, hivyo tunatoa shukurani njema kwa hawa wote na kwa wasomi na wahakiki kwa kila mmoja miongoni mwao kupitia sehemu ya tafiti hizi na kutoa mchango wao wa thamani kuhusu tafiti hizi.

Na sote tunategemea na kutaraji kuwa tutakuwa tumetoa kile tulichokiweza katika juhudi za kutekeleza baadhi ya wajibu tulionao mbele ya ujumbe wa Mtukufu Mola wetu Mlezi ambaye alimtuma Mtume Wake na uongofu na dini ya haki ili aipe ushindi dhidi ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa shahidi.

**Jumuiya ya kimataifa ya Ahlu-Bait**
**Kitengo cha utamaduni**



# UTANGULIZI

## IBARA: 'HAYYA'ALA KHAYRIL A'MAL KATIKA ADHANA'

Waislamu wametofautiana katika uwekaji na uondoaji wa ibara: "*Hayya'ala khayril a'mali*" katika adhana mara mbili, baada ya kutamka: "*Ayya'lal-Falaah*."

Lipo kundi lililosema kwamba ibara: "*Hayya'ala khayril a'mali*" haisihi katika adhana nao ni Ahlu Sunna, na baadhi yao wakasema: Ni makuruhu, wakitoa sababu kwamba jambo hilo halikuthibiti kutoka kwa Mtume (s.a.w.w), na kwa hivyo kuongeza ibara hiyo katika adhana ni Makuruhu.[2]

Ahlul Bayt (a.s) na wafuasi wao wamesema: ''Ibara hiyo ni sehemu ya adhana na iqama, bila ibara hiyo haisihi adhana wala iqama, na hiyo ni hukumu ya Ijmaa (hakuna mwanachuoni aliyehitilafiana na wenzake), na hilo wamelitolea dalili ya Ijmaa,[3] na kwa kutumia ushahidi wa hadithi nyingi zilizopokewa kutoka kwa Ahlul Bayt (a.s) kuhusiana na jambo hilo, kwa mfano hadithi ambayo imepokewa na Ali na Muhammad bin Hanafiya kutoka kwa Mtume (s.a.w.w), vile vile hadithi iliyopokewa na Abu Rabii, Zurara, Fadhiil bin Yasar na Muhammad bin Mahran kutoka kwa Imam Abu Jafar Al-Baqir (a.s).

Vivyo hivyo hadithi iliyopokewa na Ibnu Sanan, Mu'ala bin Khunas, Abu Bakr Hadhrami na Kaliib Asadi, kutoka kwa Imam Abu Abdillah as-Sadiq (a.s), aidha hadithi iliyopokewa na Abu Baswiri kutoka kwa mmoja wa Maimamu kati ya hao wawili,[4] vile vile hadithi iliyopokewa na

2 *Sunan Bayhaqi* Juz. 1, Uk. 625 na *Bahrur-Raaiq* Juz. 1, Uk. 275 kutoka katika kitabu *Sharh Muhadhab*.

3 *Al-Intiswaar* Uk. 137 cha Sayyid Murtadha.

4 Yaani Imam Baqir au Imam Swadiq (a.s.).

Hayya'alla khayril A'mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:17 PM Page 3



Muhammad bin Abi Umair kutoka kwa Abu Hasan, hali kadhalika hadithi iliyopokewa na Aqrama kutoka kwa Ibnu Abbas.[5]

Kwa hivyo kulingana na tofauti iliyokuwepo kuhusiana na jambo hilo hakuna sababu inayotufanya tuache kufuata madhehebu ya Ahlul-Bayt (a.s) na wafuasi wao, na wala hatuliegemezi hilo kwa Ijmaa pekee, bali tunalikubali hilo kwa kufuata hadithi ambazo zimepokewa kutoka kwa Ahlul-Bayt (a.s) ambao wametoharishwa na Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa Qur'ani tukufu Sura 33 Aya 33, vivyo hivyo huongezewa uzito na dalili, pia ushahidi mbali mbali ambao unapatikana kwa Ahlu Sunna.

Lakini kabla ya kueleza kwa undani zaidi na kwa urefu na mapana mada hii na kubainisha dalili na ushahidi mbali mbali unaohusiana na jambo hili, hapana budi kuweka bayana suala la uanzishwaji wa adhana katika makundi mawili, na hatimaye kuunganisha pamoja mada inayohusu ibara: "*Hayya'ala khayril a'mali*" bila shaka kutokana na hilo yatagundulika mambo mengi ambayo yanafungamana na mada hii.

## NAMNA ILIVYOANZA ADHANA KWA MUJIBU WA AHLU SUNNA

Imepokewa kutoka kwa Abu Daud amesema: ''Ametuhadithia Ubad bin Musa Hatali na Zayad bin Ayub - hadithi iliyopokewa na Ubad akahitimisha - wamesema: Ametusimulia Hashim amepokea kutoka kwa Abu Bashar, amesema Ziyad: Ametupa habari Abu Bashar amepokea kutoka kwa Abu Umair bin Anas kutoka kwa baba zake wadogo anayetokana na Answari amesema: Mtume (s.a.w.w) aliitilia umuhimu sana Swala akawa anafikiria namna gani atawakusanya watu kuhusiana na Swala, akaambiwa: 'Chomeka bendera unapokaribia wakati wa Swala watu

5 *Wasail Shi'ah, Jaamiu Ahadiith Shi'ah, Biharul-Anwar* na *Mustadrak Wasail* mlango wa adhana.

watakapoiona hapo wataitana baina yao, basi hilo halikumfurahisha, mwingine akasema: 'Ipigwe tarumbeta la Mayahudi,' wala halikumpendeza hilo, mwingine akasema: 'Tugonge kengele ya Manaswara (Wakristo) yote hayo hakuyakubali.'

Abdullah bin Zayd (bin Abdi Rabih) aliondoka katika kikao kile hali ya kuwa na machungu kutokana na machungu ya Mtume (s.a.w.w), alipolala akaota adhana akasema: Akaenda kwa Mtume (s.a.w.w) na akampa habari ile akamwambia: ''Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, nilipokuwa nimelala nikajiwa na kiumbe na akanionesha namna ya kuadhini, akasema: Na Umar alikuwa amekwisha kuona hapo kabla alificha jambo hilo sasa yakaribia siku ishirini, akamuuliza: "Kitu gani kimekuzuia usinipe habari"? Akasema: Amenitangulia Abdullah bin Zayd basi nikaona haya, Mtume (s.a.w.w) akasema: "Ewe Bilal, simama na zingatia analokuamrisha Abdullah bin Zayd basi lifanye" akasema: Bilal akaadhini, Abu Bashar akasema: Akampa habari Abu Umar kwamba Maanswari wanadhania kwamba Abdullah bin Zayd lau siku hizo angelikuwa mgonjwa Mtume (s.a.w.w) angemuainisha mwadhini mwingine.

Ametusimulia Muhammad bin Mansur Tuusi, ametuhadithia Yakub, ametuhadithia Ubayy amepokea kutoka kwa Muhammad bin Is'haq, amenisimulia Muhammad bin Ibrahim bin Harithi Taymi, kutoka kwa Muhammad bin Abdillah bin Zayd bin Abdi Rabbih amesema: Amenihadithia Abu Abdillah bin Zayd amesema: ''Pindi Mtume (s.a.w.w) alipoamrisha lipigwe tarumbeta la kiyahudi ili watu wakusanyike kwa ajili ya swala alinizunguka mtu hali nikiwa nimelala akiwa amebeba kengele mkononi mwake, nikasema: Ewe Abdillah je! Unauza kengele? Akasema: 'Unataka kuifanyia nini?' Nikasema: Ili kuwaita watu kwa ajili ya Swala, akasema: 'Je! Nikujulishe kilicho bora kuliko hiyo?' Nikasema: Bila shaka nijulishe. Akasema: Sema hivi: *Allahu akbar, Allahu akbar Allahu akbar Allah akbar Ash'hadu anla Ilaha illallah, Ash'hadu anla Ilaha illallah, Ash'hadu Anna Muhammada Rasulullah, Ash'hadu anna Muhammada Rasuulullah, Hayya'ala Swalat Hayya'ala Swalaa, Hayya'alal Falah*

*Hayya'alal Falah, Allahu akbar, Allahu akbar, La Ilaha illallah.*
Akasema: Akanyamaza kidogo kisha akasema: 'Na unapoqimu kwa ajili ya Swala sema: *Allahu akbar, Allah akbar, Ash'hadu anla Ilaha illallah, Ash'hadu anna Muhammada Rasuulullah, Hayya'ala Swalat, Hayya'alal Falah, Qad Qaamat Swalat Qad Qaamati Swalat, Allahu akbar, Allahu akbar, La Ilaha illallah.*

Na nilipoamka asubuhi nikaenda kwa Mtume (s.a.w.w) nikamweleza yale niliyoyaona usingizini akasema: "Hakika hiyo ni ndoto ya kweli Mwenyezi Mungu akipenda, simama pamoja na Bilal msomee uliyoyaona usingizini na adhini, naye afanye hivyo, kwani yeye ana sauti nzuri kuliko wewe."

Nikasimama pamoja na Bilal ikawa akisema nami nasema maneno ya adhana, Umar alisikia hayo hali ya kuwa akiwa nyumbani kwake, ghafla akatoka huku akiwa anaburuza kikoi (msuli) wake akisema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, naapa kwa yule aliyekutuma kwa haki, niliona mfano aliyoyaona yeye, Mtume (s.a.w.w) akasema: "Mwenyezi Mungu ndiye anayestahili kusifiwa."[6]

## Ibn Maaja ameipokea hadithi hiyo kwa sanad mbili zifuatazo:

Ametuhadithia Abu Abiid Muhammad bin Maimuna Madani, ametuhadithia Muhammad bin Is'haq, ametuhadithia Muhammad bin Ibrahim Taimi kutoka kwa Muhammad bin Abdillah bin Zayd kutoka kwa baba yake amesema: "Mjumbe wa Mwenyezi Mungu hakupendezwa kuhusu kengele ya Manaswara akakataa, akaoneshwa Abdillah bin Zayd usingizini." Hadi mwisho.

Ametuhadithia Muhammad bin Khalid bin Abdillah Wasitwi, ametusimulia baba yangu kutoka kwa Abdul Rahmani bin Is'haq, kutoka kwa Zuhari kutoka kwa Salim kutoka kwa baba yake: "Hakika Mtume (s.a.w.w.) alii-

6 *Sunan Abu Daud* Juz. 1, Uk. 134 – 135 nambari ya hadithi 498 – 499.

waomba watu ushauri juu ya jambo ambalo litawafanya watu wakusanyike kwa ajili ya swala, wakataja Tarumbeta akalichukia kwa ajili ya Mayahudi, kisha wakataja kengele ya Manaswara akalichukia hilo kwa sababu inahusiana na Wakristo, mtu mmoja anayeitwa Abdullah bin Zayd na Umar bin Khattab waliona katika ndoto ……."

Zuhar akasema: Na Bilal akaongeza ibara: "*Aswalatu khayru minan nawm*" katika Swala ya asubuhi, Mtume (s.a.w.w) akaipasisha hiyo ….. Hadi mwisho.[7]

**Tarmidhi amepokea kwa sanad ifuatayo:**

5. Ametuhadithia Saad bin Yahya bin Said Umawi, ametusimulia baba yangu ametuhadithia Muhammad bin Is'haq kutoka kwa Muhammad bin Ibrahim Harith Taimi, kutoka kwa Muhammad bin Abdillah bin Zayd kutoka kwa baba yake amesema: Pindi tulipoamka asubuhi tulikwenda kwa Mtume (s.a.w.w) nikamwelezea habari ya ndoto …. Hadi mwisho.

6. Tirmidhi amesema: Hadithi hiyo imepokewa na Ibrahim bin Sa'ad, na imepokewa kutoka kwa Muhammad bin Is'haq hadithi ndefu, kisha Tirmidhi akaongezea kwa kusema: Na Abdillah bin Zayd ni mtoto wa Abdu Rabbih wala hatujui ametoa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) jambo lolote linalosihi isipokuwa hadithi hiyo moja inayohusu adhana, hayo ndiyo yaliyopokewa na wanahadithi kutoka katika vitabu Sahihi au vitabu sita vya Ahlu Sunna, ambavyo vina umuhimu zaidi kuliko vingene.

Kama vile Sunan Darmi au Daru Qutni, au yale anayoyaeleza Ibn Sa'ad katika kitabu chake *Twabaqaat*, na Biyhaqi katika kitabu chake *Sunan*, na kwa ajili hiyo kuna sehemu maalumu tumeyaeleza na kuyachanganua yale yaliyopokewa katika *Sunan* zilizo maarufu na yaliyopokewa katika vitabu vingine.

[7] *Sunan Ibnu Maja* Juz. 1, Uk. 233 hadithi nambari 707 mlango wa kuanza adhana.

Basi tusome Matini ya hadithi hii na Sanadi yake hadi ibainike haki, kisha tutaje hadithi zingine zilizopokewa kuhusiana na masuala mengine, tunasema: Hakika hadithi hizo hazifai hata kidogo kuzitolea dalili na hoja katika nyanja mbali mbali:

### Mosi: Hadithi hizo hazikubaliani na cheo cha Mtume (s.a.w.w):

Hakika Mola Manani amemtuma Mjumbe wake ili kusimamisha Swala pamoja na waumini katika nyakati tofauti, na muktadha wa kadhia hiyo ilipaswa afundishwe na Mola Manani namna ya kutekeleza jambo hilo, hakuna maana ya kutahayari Mtume (s.a.w.w) kwa siku nyingi au kwa muda wa siku ishirini kama ilivyokuja katika hadithi ya kwanza, ambayo imepokewa na Abi Daud, naye hajui majukumu gani yaliyopo mabegani mwake, mara anapokea kutoka kwa huyu na mara nyingine kwa yule, anatumia kila njia ili aweze tu kufikia malengo yake, hali ya kuwa Mola Muumbaji kuhusu Mtume (s.a.w.w) anasema:

وَكَانَ فَضْلُ ٱللَّهِ عَلَيْكَ عَظِيمًا ﴿١١٣﴾

**"Na hakika fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yako ni kubwa." (*Sura Nisai*: 113.)**

Na makusudio ya fadhila ni elimu kutokana na fuo la maneno ya kabla yake, na anasema:

﴿ وَعَلَّمَكَ مَا لَمْ تَكُن تَعْلَمُ ﴿١١٣﴾

**"Na amekufundisha yale uliyokuwa huyajui" (*Sura Nisai*: 113.)**

Hakika Swala na funga ni miongoni mwa mambo ya kiibada na sio kama vile vita na mapigano ambayo huenda Mtume (s.a.w.w) alikuwa akiomba ushauri kutoka kwa Masahaba wake, na ushuauri wake haukuwa kwamba hajui namna ya kupigana au kutojua linalofaa, bila shaka ushauri wake ulikuwa kwa ajili ya kuvuta nyoyo zao kama anavyosema Mola Muumba:

Hayya'alla khayril A'mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:17 PM Page 8



﴿ وَلَوْ كُنتَ فَظًّا غَلِيظَ ٱلْقَلْبِ لَٱنفَضُّوا۟ مِنْ حَوْلِكَ ۖ فَٱعْفُ عَنْهُمْ وَٱسْتَغْفِرْ
لَهُمْ وَشَاوِرْهُمْ فِى ٱلْأَمْرِ ۖ فَإِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى ٱللَّهِ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلْمُتَوَكِّلِينَ ﴾

**"Na kama ungelikuwa mkali mshupavu wa moyo wangekukimbia basi wasamehe na waombee msamaha na ushauriane nao katika mambo, na unapoazimia basi mtegemee Mwenyezi Mungu hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wenye kumtegemea." (*Surat Aali Imran*: 159.)**

Je! Sio jambo la kipuuzi katika mambo ya dini chanzo chake kiwe ni ndoto na yale ayaonayo mtu wa kawaida usingizini? na je! Adhana na iqaama si katika mambo ya kiibada ambayo yana umuhimu mkubwa?!!

Hilo linatufanya na kutusukuma kusema kwamba ndoto kuwa ni chanzo cha kuanzishwa adhana ni jambo la uongo na kumsingizia Mtume (s.a.w.w), na la karibu sana ni kule kuona kwamba Amumah, Abdullah na Ibnu Zayd hao ndiyo ambao walioeneza ndoto hiyo na kuipamba kwa lengo la kupata fadhila familia zao na makabila yao, aidha kutumia mlolongo wa wapokezi wa uzushi, kwa hivyo tunaona katika baadhi ya vitabu ambavyo ni *Musnad* vinaeleza kwamba ukoo wa baba zake wadogo ndiyo wapokezi wa hadithi hiyo, na mtu ambaye ameitegemea na kuwakumbatia hao sio kwa kingine isipokuwa kutokana na dhana nzuri kwa watu hao.

**Pili: Hakika hadithi zote zinapingana kiasili:**

Hakika hadithi ambazo zinaelezea kuanza adhana, zinapingana kidhati na asili katika nyanja mbali mbali kama ifuatavyo:

Hakika muktadha wa hadithi ya kwanza (hadithi ya Abi Daudi) kwamba Umar bin Khattabi aliona katika ndoto kabla ya Abdillah bin Zayd kabla ya kupita siku ishirini, lakini muktadha wa hadithi ya nne (hadithi ya Ibnu Maaja) ni kwamba ameona katika usiku huo huo ambao ameona Abdillah

Hayya'alla khayril A'mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:17 PM Page 9



bin Zayd.

Hakika uono wa Abdillah bin Zayd ni chanzo cha kuanzishwa adhana na kitendo cha Umar bin Khattabi kwenda kwa Mtume (s.a.w.w) pindi aliposikia adhana na kusema: Naye vile vile ameona ndoto hiyo usiku huo, hakusema kwa sababu aliona haya.

Kwa hakika mwanzilishi wa hilo ni Umar bin Khattabi, sio ndoto yake kwa sababu yeye ndiye ambaye aliyebuni wito wa swala ambao ni ibara nyingine ya adhana.

Tirmidhi amepokea katika kitabu chake *Sunan* akasema: Pindi Waislamu walipofika Madina…. hadi aliposema: Na baadhi yao wakasema: Wawe wanapiga ngoma kama vile ngoma ya Mayahudi. Akasema: Umar bin Khattabi akasema: Je! Hampeleki mtu anadi Swala? Akasema: Mtume (s.a.w.w) akasema: "Ewe Bilal simama nadi Swala" yaani adhini. Ndio Ibnu Hajar amefasiri wito wa Swala hapo kuwa ni (*Swalat Jamia*)[8] na hakuna dalili kuhusiana na tafsiri hiyo.

Hakika mwanzo na chimbuko la sheria ni Mtume (s.a.w.w). Bayhaqi amepokea: ….. basi wakasema wapige ngoma au wawashe moto, hapo akaamrishwa Bilal aadhini kila kipengele aseme mara mbili na mara moja katika iqama. Akasema: Bukhari ameipokea hadithi hiyo kutoka kwa Muhammad bin Abdul Wahab, na Muslim amepokea kutoka kwa Is'haq bin Ammar.[9] Pamoja na ihtilafu hizo nyingi katika kunakili vipi tuitegemee?

**Tatu: Hakika watu walioota walikuwa ni kumi na wanne na sio mtu mmoja:**

Hudhihiri kutokana na yale aliyopokea Halabi kwamba hakika watu

8 *Fat'hul-Baari* Juz. 2, Uk. 81 chapa ya Darul Ma'rifa, cha Ibnu Hajar.

9 *Sunanul-Bayhaqi* Juz. 1, Uk. 608.

walioota na kuona usingizini namna ya adhana hakuwa mtoto wa Zayd na Umar pekee, bali alidai hilo Abdullah Abu Bakr kwamba yeye naye aliona waliyoyaona hao wawili. Na ilisemwa: Jambo hilo walidai watu saba miongoni mwa Answar, na ilisemwa: Ni watu kumi na wanne.[10]

Wote walidai wameona usingizini jinsi ya kuadhini, na kwamba hiyo sio sheria iliyotoka kwa Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake, kwa hivyo ikiwa sheria na hukumu zinatokana na ndoto na njozi za watu, basi ni fedheha na pigo kubwa katika Uislamu!

Ni dhahiri shahiri kwamba Mtume (s.a.w.w) anapokea sheria za dini ya Uislamu kutokana na Wahy (Ufunuo) na sio kutokana na ndoto za watu.

**Nne: Ukinzani baina ya aliyoyanukuu Bukhari na yale ya wengine:**

Hakika *Sahih Bukhari* imeeleza dhahiri kwamba Bwana Mtume (s.a.w.w) katika kikao cha mashauriano alimwamrisha Bilal anadi swala na Umar akiwa amehudhuria kikao kile pindi amri hiyo ilipotolewa, na hakika imepokewa kutoka kwa mtoto wa Umar amesema: "Waislamu walipowasili Madina walikusanyika wakijiandaa kwa ajili ya swala, siku moja hakuwepo mnadi swala wakazungumza kuhusiana na jambo hilo baadhi yao wakasema: "Chukueni kengele mgonge mfano wa kengele ya Manaswara (wakristo) na wengine wakasema: Chukueni Pembe mpige kama vile Pembe ya Mayahudi." Umar akasema: "Je! Kwa nini hamtumi mtu ili aadhini kwa ajili ya Swala?" Mtume (s.a.w.w) akasema: "Ewe Bilal simama unadi swala"[11]

Na ubainifu wa hadithi za ndoto: Hakika Mtume (s.a.w.w) alimwamrisha Bilal anadi swala wakati wa alfajiri, pindi mtoto wa Zayd alipomweleza

10 *Siiratun-Nabawiyya* Juz. 2, Uk. 95 cha Halabi.

11 *Sahih Bukhari* Juz. 1, Uk. 306 mlango wa kuanza adhana chapa ya Darul Qalam Lebanon.

Hayya'alla khayril A'mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:17 PM Page 11



ndoto hiyo, baada ya mashauriano usiku, na wala Umar hakuhudhuria katika kikao kile isipokuwa aliposikia adhana, naye akiwa nyumbani kwake akatoka hali akiwa anaburuza nguo yake na huku akisema: "Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu naapa kwa yule ambaye aliyekutuma kwa haki, nimeona mfano wa aliyoyaona."

Na sisi hatuwezi kuyachukua yale aliyoyaeleza Bukhari kuhusiana na adhana kuwa ni tamko *Swalat Jamia*, na kuchukua zile hadithi za ndoto kuwa zahusiana na adhana, kwani amezikusanya bila ushahidi, hilo la kwanza, na lau kama Mtume (s.a.w.w) alimwamrisha Bilal ainue sauti ya juu (apaze sauti) kwa tamko *Swalat Jamia* kingeondoa utata huo, hilo la pili, na tahayuri hususan ingetoweka iwapo angelikariri na kurudufu ibara *Swalat Jamia*, kwa hivyo utata na tahayuri ungelitoweka kabisa kuhusiana na mada hii. Na hiyo ndiyo ilivyo dalili ya kwamba hakika amri yake ya kutaka inadiwe Swala, ilikuwa iadhiniwe adhana hii ya kisheria.[12]

Mitazamo hiyo minne huturejesha katika kudurusu madhumuni ya hadithi, na kwa hivyo yatosheleza kabisa kukanusha utegemezi wa hadithi hizo. Ni jukumu lako kudurusu kwa makini sanadi zake moja baada ya nyingine, ni dhahiri sanadi zote hizo hakuna hata moja iliyokwenda moja kwa moja mpaka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w), aidha mpokezi wa hadithi hizo hajulikani, au ni mtu ambaye hana sifa ya kuwa mpokezi wa hadithi, au mdhaifu na mwenye kupuuzwa, kwa hivyo ni juu yako kupambanua hayo kulingana na ubainifu uliyotangulia.

**Ama hadithi ya kwanza ambayo ameipokea Abu Daudi ni dhaifu:**

1. Mlolongo wa wapokezi wa hadithi unaishia kwa mtu asiyejulikana au kwa watu wengi ambao hawajulikani, kutokana na maneno yake kwamba: Baba zake wadogo wanaotokana na Answari.

12 *Naswu Wal-Ijtihad* Uk. 200 chapa ya Us'wat cha Sharaf Dini.

2. Imepokewa kutoka kwa Amumah Abu Umair bin Anas, anamweleza Ibnu Hajar anasema: "Amepokea kutoka kwa ami zake watokanao na Maanswari miongoni mwa Masahaba wa Mtume (s.a.w.w) Hadithi inayohusu na kuona mwezi mwandamo na adhana."

Na Ibn Sa'ad akasema: "Alikuwa mkweli na mwaminifu na alikuwa ana hadithi chache."

Ibnu Abdul Barri amesema: "Hajulikani wala hadithi anayopokea haifanywi hoja."[13]

Mazzi amesema: "Haya ndiyo aliyosimulia katika maudhui mbili, kuona mwezi mwandamo na adhana, haya ndio yote aliyonayo kwao."[14]

**Ama hadithi ya pili: Imekuja katika sanadi yake mtu ambaye hafai kutolewa hoja, zipo nadharia kadhaa nazo ni:**

Muhammad bin Ibrahim bin Harith bin Khalid Taimi: Abu Abdillah aliyefariki mwaka 120 A.H.

Abu Jafar Aqil amesema kutoka kwa Abdullah bin Ahmad bin Hanbali, amesema: Nimemsikia baba yangu - akamtaja Muhammad bin Ibrahim Taimi Madani – akasema: Katika hadithi yake kuna kitu (jambo), hupokea hadithi zisizofaa au zenye kuchukiza.[15]

Muhammad bin Is'haq bin Yasar bin Khiyar, hakika Ahlu Sunna hadithi alizozipokea yeye hawazifanyi hoja, japokuwa yeye ndiye msingi wa kitabu (*Siirat Ibn Hisham*).

---

13 *Tahdhibut-Tahdhib* Juz. 12, Uk. 188 cha Ibnu Hajar nambari ya hadithi 867.

14 *Tahdhibul-Kamal* Juz. 34 Uk. 142 nambari ya hadithi 7545 cha Jamal Dini Mazzi.

15 *Tahdhibul-Kamal* Juz. 24, Uk. 304.

Ahmad bin Abi Haythama amesema: "Yahya bin Mu'in aliulizwa kuhusiana na mtu huyo akasema: ….. ni mtu dhaifu kwangu, mwenye matatizo na hana uwezo."

Abu Hasan Maimun akasema: "Nilimsikia Yahya bin Mu'in anasema: Muhammad bin Is'haq ni mdhaifu. Aidha Nisaai akasema: Ni mtu asiye na uwezo wa kupoea hadithi."[16]

Abdullah bin Zayd ni mpokezi wa hadithi, na yakutosha yale yenye kumhusu yeye kwamba ana hadithi chache sana, Tirmidhi akasema: "Hatujui kutoka kwake kitu chochote kilichokuwa sahihi alichopokea kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) isipokuwa hadithi ya adhana." Hakim akasema: Ni sahihi kuwa yeye aliuawa huko Uhud, na riwaya zote kutoka kwake zimekatwa mlolongo wa wapokezi. Ibnu Adiy amesema: Hatujui chochote kilichotoka kwake kilicho sahihi ila Hadithi ya Adhana.[17]

Na Tirmidhi amepokea kutoka kwa Bukhari: "Hatujui Hadithi yake ila ya Adhana."[18]

Hakim akasema: "Abdillah bin Zayd ndiye ambaye aliona adhana katika ndoto, adhana ambayo wanavyuoni wa kiislamu wamekubaliana juu ya hilo, wala haikuelezwa katika *Sahih* mbili kutokana na kuwepo Ihtilafu kati ya wenye kunakili katika sanadi zake (Mlolongo wa wapokezi)."[19]

Na ama hadithi ya tatu: Hakika imemjumuisha katika sanadi yake Muhammad bin Is'haq bin Yasar na Muhammad bin Ibrahim Taimi, na hakika umeshakwisha kutambua hali za hao wawili kama ulivyojua kwamba hakika Abdullah bin Zayd alikuwa ni mtu mwenye hadithi chache na

16 *Tahdhibul-Kamal* Juz. 24, Uk. 423 na *Tarikh Baghdad* Juz. 1, Uk. 221 – 224.

17 *As-Sunan ya Tirmidhiy* Juz. 1, Uk. 361. *Tahdhidut-Tahdhiib* cha Ibnu Hajar Juz. 5, Uk. 225.

18 *Tahdhibul-Kamal* cha Jamulud-Din Mazzi Juz. 14, Uk. 514.

19 *Mustadrak Hakim* Juz. 3, Uk. 336.

Hayya'alla khayril A'mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:18 PM Page 14



hadithi zote zilizopokewa na yeye zina mapungufu.
**Ama hadithi ya nne imekuja katika sanadi yake watu wafuatao:**

Abdul Rahman bin Is'haq bin Abdullah Madani: Yahya bin Said Qatwani amesema: "Niliuliza Madina kuhusu yeye, sikuwaona wao wakimtukuza yeye, vivyo hivyo amesema Ali bin Madiini."

Vile vile Ali amesema: "Nimemsikia Sufyan - na akamuuliza kuhusiana na Abdul Rahman Ibn Is'haq - amesema: Alikuwa mtu wa Qadar (majaaliwa) watu wa Madina walimtenga, akatujia sehemu tuliyokuwa tumekaa na Maqtalul-Waliid basi wala hatukukaa naye."

Abu Twalib akasema: "Nilimuuliza Ahmad bin Hambali kuhusu yeye akasema: Amepokea kutoka kwa Abu Zunad hadithi potovu." Na Ahmad bin Abdillah Ajali amesema: "Huandikwa hadithi zake lakini hafai bali ni mdhaifu." Na Abu Hatam amesema: "Huandikwa hadithi zake na hazifanywi hoja."

Bukhari akasema: "Hakuwa miongoni mwa watu ambao hutegemewa katika kuhifadhi hadithi …. wala hafahamiki mwanafunzi wake huko Madina isipokuwa Mussa Zamuii, yeye amepokea kutoka kwake hadithi katika nyanja mbalimbali, na zote zina mkanganyiko."

Na Daru Qutni amesema: "Ni mtu mdhaifu, aidha hutuhumiwa kuwa ni mtu wa Qadar, na Ahmad bin Uday amesema: Katika hadithi alizozipokea baadhi yake hukanushwa, huchukiwa na zingine hazifuatwi."[20]

Muhammadi bin Abdillah Wasitwi amesema: "Jamalud-Diin Mazzi anamueleza kwa kusema: Ibnu Mu'in amesema: Si chochote na hadithi alizozipokea kutoka kwa baba yake hazifai."

20 *Tahdhibul-Kamal* Juz. 16, Uk. 515 nambari ya hadithi 3755 cha Jamal Dini Mazzi.

Abu Hatam akasema: "Nilimuuliza Yahya bin Mu'in akasema: Ni mtu muovu na muongo, na ameeleza vitu vingi vya kupotosha," na akasema Abu Uthman Said bin Umar Burdai: Na nikamuuliza yeye - Abu Zar'aa – kuhusu Muhammad bin Khalid, akasema: Ni mtu muovu, na Ibn Haban amemuelezea katika kitabu chake *Thuqaat* na akasema: "Alikuwa akikosea na kueleza kinyume."[21]

Na Shawkani baada ya kunukuu hadithi akasema: "Na katika mlolongo wa wapokezi wake ni wadhaifu mno."[22]

**Ama hadithi ya tano imekuja katika sanadi yake watu hawa wafuatao:**

Muhammad bin Is'haq bin Yasar.
Muhammad bin Harith Taimi.
Abdullah bin Zayd.

Na umeshakwisha kujua udhaifu wa wawili wa mwanzo, na kuwa mlolongo wa wapokozi wao katika yote wanayopokea kutoka kwa wa tatu ni butu, aidha wana mapungufu makubwa, kwa hivyo inadhihirika hali ya njia ya sita, basi chunguza hilo. Hayo yapo katika baadhi ya vitabu Sahihi, ama yale yaliyomo katika vitabu vingine tunaeleza kutoka kwake yale aliyopokea Imam Ahmad, Darmi na Darul Qutni katika *Musnad* zao, Imam Malik katika kitabu chake *Muwatwau*, Ibnu Sa'ad katika kitabu chake *Twabaqaat* na Bayhaqi katika kitabu chake *Sunan* na zingatia ubainifu huu:

**1: ALIYOYAPOKEA IMAM AHMAD KATIKA MUSNAD YAKE:**

Amepokea Imam Ahmad ndoto inayohusu adhana katika *Musnad* yake kutoka kwa Abdullah bin Zayd kwa sanadi tatu. [23]

21 *Tahdhiul-Kamal* Juz. 25, Uk. 138 nambari ya hadithi 5177.
22 *Naylul-Awtar* Juz. 2, Uk. 42 cha Shawkani.
23 *Mustadrak Imam Ahmad* Juz. 4, Uk. 632 na 633 hadithi nambari 16041, 16041, 16042 na 16043. w

**i**. Yumo katika njia ya kwanza Zayd bin Haban bin Rayyan aliyefariki mwaka 203 A.H.Na walimuelezea kuwa ni mtu mwenye makosa mengi na anazo hadithi nyingi zisizojulikana upande wa njia ya upokezi wake kutoka kwa Sufyan Thauri, na Ibnu Mu'in akasema: "Hadithi ambazo hupokewa na Sufyan Thauri ni zilizogeuzwa na kubadilishwa."[24]

Vile vile njia hiyo inamjumuisha Abdullah bin Muhammad bin Abdillah bin Zayd bin Abdi Rabbih naye hana hadithi katika vitabu *Sahihi* na *Musnad* zote isipokuwa hadithi moja tu, nayo ni hiyo ambayo inaelezea ubora wa familia yake, na kwa ajili hiyo hupungua utegemezi wake.

**ii**. Yumo katika njia ya pili Muhammad bin Is'haq Yasar ambaye umeshakwisha mtambua hapo kabla.

**iii**. Yumo katika njia ya tatu Muhammad bin Ibrahim Harith Taimi, ukiongezea Muhammad bin Is'haq, na huishia kikomo kwa Abdullah bin Zayd ambaye ana hadithi chache sana.

Na imekuja katika hadithi ya pili baada ya kutaja ndoto na ufundishaji wa adhana kwa Bilal: "Hakika Bilal alikwenda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akamkuta amelala akaita kwa sauti ya juu: "*Aswalatu khayru minan naum*" yaani swala ni bora kuliko usingizi, basi ibara hiyo ikaingizwa katika adhana ya swala ya alfajiri."

## 2. ALIYOYAPOKEA DARMI KATIKA *MUSNAD* YAKE:

Amepokewa Darmi ndoto inayohusu adhana katika kitabu chake kinachoitwa *Musnad* kwa njia kadhaa za wapokezi wa hadithi, na wote ni wadhaifu, ambao hawana hata kidogo sifa za kupokea hadithi, na zifuatazo ni

24 *Miizanul-Iitidal* Juz. 2, Uk. 100 hadithi nambari 2997 cha Dhahabi.

baadhi ya njia hizo:

1. Ametuhadithia Muhammad bin Hamiid, ametusimulia Salmah: Amenihadithia Muhammad bin Is'haq, amesema: ''Hakika Mtume (s.a.w.w.) pindi alipokuwa ……hadi mwisho.''

2. Katika njia hiyo hiyo ya wapokezi imekuja baada ya Muhammad bin Is'haq, amesema: Amenihadithia hadithi hii Muhammad bin Ibrahim bin Harith Taimi kutoka kwa Muhammad bin Abdillah bin Zayd bin Abdi Rabbih kutoka kwa baba yake.

3. Ametupa habari Muhammad bin Yahya: Ametusimulia Yakub bin Ibrahim bin Saad kutoka kwa Ibn Is'haq….. na yaliyobaki ni yale yaliyokuwepo katika njia ya pili ya wapokezi.[25]

Njia ya kwanza ni butu, ama ya pili na ya tatu yumo Muhammaad bin Ibrahim bin Harith Taimi, na umeshakwisha itambua hali yake, kama vile ulivyoitambua hali ya Ibn Is'haq.

**3. YALIYOPOKEWA NA IMAM MALIK KATIKA KITABU CHAKE *MUWATWAI*:**

Amepokea Imam Malik ndoto inayohusiana na adhana katika kitabu chake *Muwatwai* kutoka kwa Yahya, imepokewa kutoka kwa Malik, naye amepokea kutoka kwa Yahya bin Said amesema: Bwana Mtume (s.a.w.w.) alitaka zichukuliwe mbao mbili na zigongwe kwa pamoja … [26]

Na njia yake ni butu, mradi wake ni Yahya bin Said Qais ambaye alizaliwa mwaka 70 A.H. na kufariki sehemu inayoitwa Hashimiya mwaka 143 A.H.[27]

25 *Sunanud-Darmi* Juz. 1, Uk. 287 mlango wa kuanza adhana.
26 *Muwatwai* Juz. 44 mlango wa yaliyokuja katika kuanza kwa adhana cha Malik.
27 *Siiratul-A'alam Nubalaa* Juz. 5, Uk. 468 hadithi nambari 213 cha Dhahabi.

## 4. YALIYOPOKEWA NA IBN SA'AD KATIKA KITABU *TWABAQAAT*:

Ameipokea hadithi hiyo Muhammad bin Saad katika kitabu chake T*wabaqaat*[28] kwa njia butu ambazo hazikubaliki wala hazifanywi kuwa ni hoja:

**Mosi:** Njia ya wapokezi wake inaishia kwa Nafiu bin Jubair ambaye amefariki katika miaka ya 90 A.H., na imesemwa kwamba ni mwaka 99 A.H.

**Pili:** Njia ya wapokezi wake inakomea kwa Urwat bin Zubeir ambaye alizaliwa mwaka 29 A.H. na kufariki mwaka 93 A.H.

**Tatu:** Njia ya wapokezi wake inaishia kwa Zayd bin Aslam ambaye amefariki mwaka 136 A.H.

**Nne:** Njia ya wapokezi wake inakomea kwa Said bin Masiib ambaye amefariki mwaka 94 A.H. na hadi kwa Abdul Rahman bin Abu Layla ambaye amefariki mwaka 82 au 83 A.H.

Dhahabi katika wasifu wa Abdullah bin Zayd akasema: "Amehadithia kutoka kwake Said bin Masiib na Abdul Rahman bin Abu Layla - na hakumdiriki."[29]

Vile vile amepokea kwa njia ya wapokezi ufuatao: Ametusimulia Ahmad bin Muhammad bin Walid Azraqi: Ametusimulia Muslimu bin Khalid: Amenihadithia Abdul Rahim bin Umar kutoka kwa Ibnu Shihab kutoka kwa Salim bin Abdillah bin Umar kutoka kwa Abdullah bin Umar amesema: "Hakika Mtume (s.a.w.w.) alitaka afanye kitu ambacho kitawakusanya

28 *Twabaqaatul-Kubra* Uk. 342 – 247 cha Ibnu Sa'ad.

29 *Siiratul- Aalaam Nubalaa* Juz. 2, Uk. 375 hadithi nambari 79 na ufafanuzi zaidi taz. sehemu ya pili.

watu pamoja, hadi mtu mmoja miongoni mwa Maanswar aitwaye Abdillah bin Zayd alipooneshwa usingizini, aidha akaoneshwa Umar bin Khattabi usiku ule ule ….." Akaendelea hadi aliposema: "Bilal akaongeza katika adhana ya swala ya asubuhi sentensi hii "*Aswalatu khayru minan naum*" basi Mtume (s.a.w.w.) akainyamazia."

Na kwa hakika katika njia hii wamo:

Muslim bin Khalid bin Qurat. Na huitwa Ibnu Jarha. Yahya bin Mu'in amemdhoofisha. Ali bin Madiini amesema: "Yeye si lolote."

Na Bukhari akasema: "Hutupiliwa mbali hadithi aliyoipokea." Nisaai akasema: "Hakuwa mtu mwenye kuhifadhi." Na Abu Hatam akasema: "Ni mdhaifu, hadithi yake hutupiliwa mbali, hadithi aliyoipokea huandikwa lakini haifanyiwi kazi wala kutolewa hoja, hujulikana na hukanushwa."[30]

Muhammad bin Muslim bin Ubaidullah bin Abdillah bin Shihab Zuhari Madani alizaliwa mwaka 51 A.H. na kufariki mwaka 123 A.H.
Amesema Anas bin Ayadh kutoka kwa Ubaidullah bin Umar, amesema: "Nilikuwa namuona Zuhari akipewa kitabu lakini hakuwa anakisoma wala kusomewa, basi huambiwa yeye (Muhammad bin Muslim): Je! Haya tupokee kutoka kwako? naye hujibu ndio."

Ibrahim bin Abi Sufyan Qaisarani amepokea kutoka kwa Faryabi amesema: "Nimemsikia Sufyan Thauri akisema: Nilikwenda kwa Zuhari (Muhammad bin Muslim) akanipuuza, nikamwambia: 'Lau wewe ungewaendea Masheikh wetu, na wakakufanyia wewe mfano huu!' Basi akasema: 'Kama vile wewe.' hapo akaingia ndani na akatoka na kitabu akasema: 'Chukua hiki na upokee kutoka kwangu,' wala sikupokea kutoka kwake hata herufi moja."[31]

30 *Tahdhibul-Kamal* Juz. 27, Uk. 508 nadithi nambari 5925 cha Jamal Dini Mazzi.

31 *Tahdhibul-Kamal* Juz. 26, Uk. 439 – 440.

## 5: YALIYOPOKEWA NA BAYHAQI KATIKA KITABU CHAKE *SUNAN*:

Bayhaqi amepokea ndoto inayohusu adhana kwa njia za wapokezi ambazo zote hazikosi kuwa na matatizo na kasoro, na zingatia vidokezo kadhaa vya wapokezi wadhaifu waliyomo katika njia za wapokezi wake:

**Mosi:** Njia ya wapokezi inamjumuisha Abu Umair bin Anas kutoka kwa baba zake wadogo wanaotokana na Answari, na umeshakwisha mtambua Abu Umair bin Anas, Ibnu Abdul Bari amesema: "Yeye hajulikani, aidha hazitolewi hoja hadithi azipokeazo, vile vile hupokea hadithi kutoka kwa watu wasiojulikana[32] kwa kutumia jina la baba wadogo." Na hakuna dalili inayojulisha hao ni miongoni mwa Masahaba, na hata ikiwa tutajaalia kila Sahaba ni mwadilifu, na iwapo tutakubaliana na kusalenda kwamba baba zake wadogo walikuwa ni miongoni mwao, lakini yale ya Maswahaba yanayotiliwa shaka si hoja, kwa sababu hatuna yakini kama aliyapokea toka kwa masahaba.

**Pili:** Njia ya wapokezi inajumuisha watu ambao hawafai wala hawatolewi hoja nao ni:

1. Muhammad bin Is'haq bin Yasar.
2. Muhammad bin Ibrahim bin Harith Taimi.
3. Abdullah bin Zayd.

Na hakika wote hao umeshakwisha utambua udhaifu wao.

**Tatu:** Katika njia ya wapokezi yumo Ibnu Shihab Zuhari, imepokewa kutoka kwa Said bin Masiib, amefariki mwaka 94 A.H kutoka kwa Abdullah bin Zayd, na huyo umeshakwisha mtambua kuwa hajamuona Abdullah bin Zayd.[33]

32 *Tahdhibut-Tahdhib* Juz. 12, Uk. 188 hadithi nambari 867 cha Ibnu Hajar.
33 *Sununul-Bayhaqi* Juz. 1, Uk. 575 hadithi nambari 1837.

## 6. YALIYOPOKEWA NA DARUL QUTNI:

Darul Qutuni amepokea ndoto inayohusu adhana kwa njia ya wapokezi wa hadithi na huu ndiyo ubunifu wake:

1. Ametuhadithia Muhammad bin Yahya bin Murdaas: Ametusimulia Abu Daud: Ametuhadithia Uthman bin Abu Shayba: Ametusimulia Hamad bin Khalid Amru, amepokea kutoka kwa Muhammad bin Abdullah kutoka kwa ami yake Abdullah bin Zayd.

2. Ametuhadithia Muhammad bin Yahya amesema: Ametuhadithia Abu Daud: Ametusimulia Ubaidullah bin Umar: Ametuhadithia Abdul Rahman bin Mahdi: Ametuhadithia Muhammad bin Amru: Amesema: Nimemsikia Abdullah bin Muhammad akisema: Alikuwa babu yangu Abdullah bin Zayd …Akasimulia habari hii.[34]

Hakika zimekusanya njia mbili hizi za wapokezi jina la Muhammad bin Amru, naye ni asiyekubalika baina ya Answari, ambaye hana katika vitabu *Sahih* na *Musnad* isipokuwa hadithi hiyo pekee. Dhahabi amesema: ''Haeleweki na hajulikani.'' Hali kadhalika Muhammad bin Amru Abu Sahil Answar ambaye Yahya Qatani amesema: ''Ni mdhaifu,'' vivyo hivyo Ibnu Mu'in na Ibnu Uday wamesema hivyo.[35]

3. Ametuhadithia Abu Muhammad bin Saad: Ametusimulia Hasan bin Yunus: Ametuhadithia As'wad bin Aamir: Ametuhadithia Abu Bakar bin Ayshi kutoka kwa Asmash, kutoka kwa Amru bin Murrat, kutoka kwa Abdul Rahman bin Abi Layla, kutoka kwa Maadh bin Jabal, amesema:

34 *Miizanul-I'itidal* Juz. 3, Uk. 674 hadithi nambari 8017 na 8018 cha Dhahabi, *Tahdhibul-Kamal* Juz. 26, Uk. 220 hadithi nambari 5516 cha Jamal Dini Mazzi, na *Tahdhibut-Tahdhibu* Juz. 9, Uk. 378 hadithi nambari 620 chapa ya Daru Swadir, cha Ibnu Hajar.

35 *Sunan*, Juz. 1, Uk. 242 hadithi nambari 31 cha Darul Qutni.

> Mtu mmoja miongoni mwa Maanswar, yaani Abdullah bin Zayd alisimama mbele ya Mtume (s.a.w.w.) akasema: ''Hakika mimi nimeota usingizini…..[36]

Na hii ndio njia iliyo butu, kwani Maadhi bin Jabal alifariki mwaka 20 A.H. au 18 A.H. na Abdul Rahmani bin Abi Layla amezaliwa mwaka 17 A.H. Zaidi ya hapo ni kwamba Darul Qutni alisema Abdul Rahman ni mtu mdhaifu na akasema: "Mdhaifu wa hadithi ana hifadhi mbaya, naye Ibnu Abi Layla usikivu wake kutoka kwa Abdullah bin Zayd haujathibiti."[37]

Mpaka hapa tumefikia hatamu ya maelezo yetu, bila shaka imebainika, na kwa hivyo hatuwezi sema: Hakika chanzo cha adhana na kufanywa kuwa sheria ni ndoto ya Abdullah bin Zayd au ndoto ya Umar bin Khattabi na wasio kuwa hao miongoni mwa watu waliyo kuweko wakati ule, na kwa hakika hadithi hizo zinapingana kiasili na dhati yake, hazikutimia katika njia ya wapokezi wake, bali ni butu, siyo kamilifu, aidha hazithibitishi lolote, ukiongezea yale tuliyoyataja mwanzoni mwa mada kutokana na jambo hilo kupingwa kiakili.

## NAMNA ILIVYOANZA ADHANA KWA MUJIBU WA AHLUL BAYT (A.S):

Tunapozingatia hadithi ambazo zimepokewa kutoka kwa Ahlul Bayt (a.s) kuhusiana na chimbuko la adhana hatuoni ndani yake jambo lililohadharishwa kama lile la maelezo yaliyotangulia, bali yote yanasigana na cheo na daraja la Mtume (s.a.w.w.).

Imepokewa kutoka kwa Abu Abdillah Swadiq (a.s) amesema: ''Pindi Malaika Jibril (a.s) alipoteremka kwa Mtume (s.a.w.w.) akiwa ameleta

36 *Sunan* Juz. 1, Uk. 242 hadithi nambari 31 cha Darul Qutuni.

37 *Wasail* Juz.. 4, Uk. 612 mlango wa adhana na iqaama hadithi nambari 2.

Hayya'alla khayril A'mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:18 PM Page 23



adhana, kichwa chake (s.a.w.w.) kilikuwa juu ya paja la Ali, Jibril (a.s) akaadhini na akakimu. Na pindi Mtume (s.a.w.w) alipozinduka akasema: 'Ewe Ali je! Umesikia?' Akajibu: 'Ndiyo,' akasema: 'Je! Umehifadhi?' Akajibu: 'Ndiyo,' akasema: 'Mwite Bilal na mfundishe.' Ali (a.s) akamwita Bilal akamfundisha.[38]

Tofauti iliyopo kati ya hadithi mbili ni kuwa katika hadithi ya kwanza Jibril (a.s) alikuwa na lengo la kutekeleza Swala ya Sunna mingoni mwa Sunna, tofauti na hadithi ya pili ambayo lengo ilikuwa ni kumbainishia na kumfundisha Sunna Mtume (s.a.w.w,), na kwa hivyo tunamuona Mtume (s.a.w.w) akimwambia Ali bin Abi Twalib (a.s): "Mwite Bilal na amfundishe hivyo."

Nadharia hiyo inaungwa mkono na hadithi nyingi ambazo amezitaja Asqalaani na akajadili njia zake na wapokezi wake, akasema:

"Zimepokewa hadithi chungu nzima zinazojulisha namna adhana ilivyoanzishwa, kwa hakika ilianzishwa Makka kabla Mtume (s.a.w.w) hajahamia Madina, miongoni mwa hadithi hizo ni: Twabarani amepokea kwa njia ya Salum bin Abdillah bin Umar kutoka kwa baba yake amesema: Pindi Mtume (s.a.w.w) alipopelekwa Miraji Mwenyezi Mungu alimfunulia adhana, alirejea kutoka Miraji akamfundisha Bilal, na katika mlolongo wa wapokezi wake ni Twalha bin Zayd, naye ni mwenye kuachwa."

Hadithi hizo amezinukuu Askalani ambazo zinajulisha wazi mtazamo wa madhehebu ya Ahlul Bayt (s.a) kuhusiana na uanzishwaji wa adhana, na kukanusha vikali dhana kwamba asili na mwanzo wake ni ndoto ya Abdullah bin Zayd au Umar bin Khattabi.

Kwa hakika imepokewa kutoka kwake (a.s) kuwa: 'Hakika yeye aliwalaani watu ambao wamedhani kwamba Mtume (s.a.w.w) amechukua adhana

38 *Wasail* Juz.. 4, Uk.. 612 mlango wa adhana na iqaama hadithi nambari 2.

kutoka kwa Abdullah bin Zayd, akasema: "Wahyi unateremshwa kwa Nabii wenu na mnadhani kuwa amechukua adhana kutoka kwa Abdullah bin Zayd?!!"[39]

1. Askalan ameeleza kutoka kwa Bazazi kutoka kwa Ali (a.s), amesema: ''Pindi Mwenyezi Mungu alipotaka amfundishe Mjumbe wake adhana alijiwa na Jibril akiwa na mnyama anayeitwa Buraq basi akampanda.''[40]

2. Imepokewa kutoka kwa Abu Ja'far (a.s) katika Hadithi ya Miraji, amesema: Kisha akamwamrisha Jibril (a.s), basi akaadhini mara mbili kila ibara na mara mbili katika iqaama, hapo akasema katika adhana: *"Hayya'ala khayril a'mali"* kisha Mtume (s.a.w.w) akatangulia mbele akawaswalisha watu.[41]

3. Imepokewa kutoka kwa Abu Abdullah (a.s) amesema: ''Pindi Mtume (s.a.w.w) alipopelekwa Miraji ulipowadia wakati wa Swala Jibril (a.s) akaadhini.''[42]
4. Amepokea Abdul Razzaq kutoka kwa Muamar kutoka kwa Ibnu Hamad, kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake, kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) katika hadithi ya Miraji, amesema: "Kisha Jibril akasimama akaweka kidole chake cha shahada cha kulia sikioni mwake akaadhini mara mbili, na mwisho wa adhana akasema: *"Hayya'ala khayril a'mali"* mara mbili.[43]

39 *Fat-hul-Baari Fii Sharh Bukhari* Juz. 2, Uk. 78 Darul Ma'arifa Lebanon.

40 *Wasailus-Shi'a* mlango 19 hadithi nambari 1, kati ya milango ya adhana na iqaama cha Muhammad bin Hasan Hurru Aamili.

41 *Wasailus-Shi'a* mlango 19 hadithi nambari 1kati ya milango ya adhana na iqaama cha Muhammad bin Hasan Hurru Aamili.

42 *Sa'adus-Su'ud* Uk. 100; *Biharul-Anwar* Juz. 81, Uk. 107 na *Jaamiul-Ahadiith Shi'ah* Juz. 2 Uk. 221.

43 *Sunanul-Bayhaqi* Juz. 1, Uk. 624 hadithi nambari 1991.

**UTHIBITISHO WA IBARA*: "HAYYA'ALA KHAYRIL A'MALI*":**

Dalili ambazo zinatufanya sisi tushikamane na ibara: *"Hayya'ala khayril a'mali"* kuwa ni sehemu ya adhana na iqama, kwa hivyo adhana na iqama haitosihi bila kusomwa ibara hiyo, ni kama ifuatavyo:
Mosi: Maandiko yaliyopatikana kutoka kwa Masahaba wa Mtume (s.a.w.w.): Kutokana na hayo tunatoa mfano: Yale yaliyopo katika njia sahihi za wapokezi wa hadithi kutoka kwa baadhi ya Masahaba wa Mtume (s.a.w.w.), mfano:

**Abdullah bin Umar.**
**Suhail bin Haniif.**
**Bilal.**
**Abu Mahdhura.**
**Ibnu Abi Mahdhura.**
**Zayd bin Arqam.**

**Yaliyokuja kutoka kwa Abdullah bin Umar:**

Hakika imepokewa hivi:
i. Kutoka kwa Naafiu amesema: Alikuwa Ibnu Umar wakati fulani pindi anaposema: *"Hayya'alal Falaah"* baada ya ibara hiyo husema: *"Hayya'ala khayril Amali."*[44]

ii. Imepokewa kutoka kwa Layth bin Saad kutoka kwa Naafiu amesema: Alikuwa mtoto wa Umar haadhini pindi akiwa safarini isipokuwa akisema: *"Hayya'la khayril a'mali."*[45]

44 *Sunanul-Bayhaqi* Juz. 1, Uk. 624 hadithi nambari 1991.
45 *Sunanul-Bayhaqi* Juz. 1, Uk. 624 hadithi nambari 1991. *Dalailus-Swiduq* Juz. 3, Uk. 100 sehemu ya pili kutoka *Mabadiu Fiqhul-Islami* Uk. 38 cha Arafi kutoka *Sharhut-Tajriid* na imepokewa na Ibn Abi Shayba ameinukuu katika kitabu *Shifaa* na ipo katika kitabu *Jawahirul-Akhbar Wal-Athaar* kimetolewa kutoka kitabu *Lujnatul-Bahruz-Zikhaar* Juz. 2, Uk. 192 cha Swa'adi.

iii. Na imepokewa kutoka kwa Layth bin Sa’ad kutoka kwa Naafiu amesema: Huenda mtoto wa Umar akawa ameongeza katika adhana yake kipengele: *“Hayya’ala khayril a’mali.”*[46]

iv. Vivyo hivyo amepokea Nasiir bin Dhu’uluq kutoka kwa mtoto wa Umar, na akasema: Alifanya hivyo (mtoto wa Umar) akiwa safarini.[47]

v. Abdul Razzaq amepokea kutoka kwa Muammar kutoka kwa Yahya kutoka kwa Abu Kathiri kutoka kwa mtu mmoja amesema: ‘’Hakika mtoto wa Umar alipokuwa anaadhini baada ya kusema: *“Hayya’alal falaah”* husema: *“Hayya’ala khayril a’mali”* kisha husema: *“Allahu akbar Allahu akbar, La Ilaha Illallah.”*[48]

Hali kadhalika hadithi hiyo ameipokea Ibnu Abi Shayba[49] kupitia njia ya Ibnu Ajalan na Ubaidullah kutoka kwa Naafiu kutoka kwa Ibnu Umar.

**Yaliyopokewa kutoka kwa Sahal bin Haniif:**

i. Amepokea Bayhaqi kwamba aliyesoma maneno: *“Hayya’ala khayril a’mali”* katika adhana, na amepokea kutoka kwa Abi Umama ni Sahal bin Haniif.[50]

ii. Amenukuu Ibnu Waziri kutoka kwa Muhibbu Twabari Shaafi katika kitabu chake *Ihkamul Ahkam*: “… Alya’ala aliitamka *(Hayya’ala khayril a’mali*): Imepokewa kutoka kwa Swidiqah bin Yasar, kutoka kwa Abu Amumah, Suhal bin Haniif, amesema: Pindi akiadhini alikuwa akisema: “*Hayya’ala khayril a’mali*” hadithi hiyo ameeleza

46 *Sunanul-Bayhaqi* Juz. 1, Uk. 625 chapa ya Darul Kutubul Ilmiya - Lebanon.

47 *Sunanul-Bayhaqi* Juz. 1, Uk. 460 chapa ya Darul Kutubul Ilmiya - Lebanon.

48 *Sunanul-Bayhaqi* Juz. 1, Uk. 145 na pambizo ya *Muswannaf* cha Abdul Razzaq Juz. 1, Uk. 460 kutoka kwake.

49 *Sunanul-Bayhaqi* Juz. 1, Uk. 425.

50 *Dalailus-Swiduq* Juz. 2, Uk. 100 sehemu ya 2 kutoka *Mabadiu Fiqhul-Islami* Uk. 38 chapa ya mwaka 1354 A.H.

Said bin Mansur.[51]

**Yaliyopokewa kutoka kwa Bilal ni kama ifuatavyo:**

1. Imepokewa kutoka kwa Abdullah bin Muhammad bin Ammar, kutoka kwa Ammar na Umar watoto wa Hafswa bint Umar, kutoka kwa baba zao kutoka kwa mababu zao, kutoka kwa Bilal amesema: Kwa hakika yeye alikuwa akinadi swala ya asubuhi akisema: *"Hayya'ala khayri a'mali"* Mtume (s.a.w.w) akamuamrisha aweke sehemu yake: *"Asswalatu khyru minan naumi"* na akaacha maneno *"Hayya'al khayril a'mali."*[52]

Lakini mwisho wa hadithi kuna mushkeli, na hilo ni kwa sababu ya ibara: *"Asswalatu khayru minan naumi"* imeongezwa katika adhana baada ya kufariki bwana Mtume (s.a.w.w), kama zilivyoeleza bayana hadithi mbali mbali, hapa tunaziashiria baadhi tu kuhusiana na mada hii.[53]

Bilal alikuwa akiadhini kwa swala ya asubuhi akisema: *"Hayya'ala khayril a'mali."*[54]

---

51 *Majmauz-Zawaid* Juz. 1, Uk. 33 kutoka kitabu *Al-Kabiir* cha Twabarani; *Muswannaf* Juz. 1, Uk. 460 hadithi nambari 1786 cha Abdul Razzaq, *Sunanul-Bayhaqi* Juz. 1, Uk. 625 hadithi nambari 1994, *Muntakhabul-Kanzu* pambizo ya *Musnad* Juz. 3, Uk. 276 kutoka kwa Abu Sheikh katika kitabi Adhan na *Dalailus-Swiduq* Juz. 2, Uk. 99 sehemu ya 2.

52 *Muwatwau* cha Malik Uk. 46. *Sunanud-Darul Qutuni*. *Muswannaf* Juz. 1, Uk. 474 na 475 hadithi 1994 na nambari 1827, 1829 na 1832 cha Abdul Razzaq na *Mutakhab* pambizo ya *Musnad* Juz. 3, Uk. 278 na humo ipo ibara: Iwapo atasema hiyo ni bida'a. Na Tirmidhi, Abu Daud na wengineo.

53 *Muntakhab Kanzul-Ummal* pambizo ya *Musnad* Juz. 3, Uk. 276 na *Dalailus-Swiduq* Juz. 3, Uk. 99 sehemu ya 2 kutoka *Kanzul-Ummal* Juz. 4, Uk. 266.

54 Bahruz-Zikhar Juz. 2, Uk. 192; *Jawahir Akhbar Wal-Athaar* pambizoni, ukurasa huo huo.

**Yaliyopokewa kutoka kwa Abu Mahdhura:**

1. Amepokea Muhammad bin Mansuri katika kitabu chake *Jaamiu* kwa njia ya wapokezi wake kutoka kwa wapokezi walioridhiwa, kutoka kwa Abu Mahdhura mmoja wa waadhini wawili wa Mtume (s.a.w.w), amesema: "Mtume (s.a.w.w.) aliniamrisha niseme katika adhana: *"Hayya'ala khayri a'mali."*[55]

2. Imepokewa kutoka kwa Abdul-Azizi bin Rafii kutoka kwa Abu Muhdhura amesema: Pindi nilipokuwa kijana Mtume (s.a.w.w) aliniambia: "Unapoadhini mwisho weka maneno *"Hayya'ala kahyril a'mali.*"[56]

**Yaliyopokewa kutoka kwa mtoto wa Abu Mahdhura:**

Katika kitabu *Shifaa* imepokewa hadithi kutoka kwa Hadhiil bin Bilal Madaini, amesema: ''Nilimsikia mtoto wa Abu Mahdhura akisema katika adhana: *"Hayya'alal falaah, Hayya'ala khayril a'mali*."[57]

**Yaliyopokewa kutoka kwa Zayd bin Arqam:**

Hakika imepokewa kwamba yeye aliadhini kwa kusema maneno haya: *''Hayya'ala khayril a'mali*."[58] Halabi amesema: "….na imenukuliwa kutoka kwa mtoto wa Umar, na kutoka kwa Ali bin Husein (a.s.), hakika hao wawili walipokuwa wanaadhini baada ya kusema: *"Hayya'alal falaah*, walisema: *Hayya'ala khayril a'mali.* "[59]

55 *Miizanul-I'itidal* Juz. 1, Uk. 139 cha Dhahabi na *Lisanul-Miizan* Juz. 1, Uk. 268 cha Askalani.

56 *Miizanul-I'itidal* Juz. 1, Uk. 139 cha Dhahabi na *Lisanul-Miizan* Juz. 1, Uk. 268 cha Askalaani.

57 *Imam Swadiq Wal-Madhahibu Arba'at* Juz. 5, Uk. 283.

58 *Siiratul-Halabiya* Juz. 2, Uk. 98 mlango wa adhana kimesambazwa na Maktabat Islamiya.

59 *Dalailus-Swiduq* Juz. 3, Uk. 100 sehemu ya 2 kutoka kitabu *Mabadiu Fiqhul-Islami* Uk. 37 cha Arafi chapa ya mwaka 1354 A.H., na kitabu *Muhalla* Juz. 3, Uk. 160.

Na Alaud-Dini Hanafii katika kitabu chake *Talwiihu* katika sherehe ya *Jaamiu Swahih* akasema: ''Na ama kuhusu maneno "*Hayya'ala khayril a'mali*" ametaja Ibnu Hazim kwamba Abdullah bin Umar ameikubali na akasema ni sahihi, vivyo hivyo imepokewa kutoka kwa Abu Amumah Suhal bin Haniif, kwamba wawili hao walikuwa wakisema: *"Hayya'ala khayril a'mali"* …kisha akasema: Na alikuwa Ali bin Husein akifanya hivyo…."[60] Vile vile alikuwa Ibnu Nabah anapoadhini akisema: *"Hayya'ala khayril a'mali."*[61]

**PILI: YALIYOPOKEWA KWA SANADI SAHIHI KUTOKA KWA AHLUL-BAYTI (A.S.):**

**Yaliyopokewa kutoka kwa Imam Ali (a.s):**

Hakika imepokewa kutoka kwake (a.s.) amesema: ''Nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akisema: ''Jueni kwamba miongoni mwa amali zenu, bora ni Swala." akamwamrisha Bilal aadhini na aseme: *Hayya'ala khayril a'mali."*

Hayo ameyaelezwa katika kitabu kiitwacho *Shifau*.[62]

**Yaliyopokewa kutoka kwa Imam Ali bin Husain (a.s.):**

i. Imepokewa kutoka kwa Hatam bin Isma'il kutoka kwa Ja'far bin Muhammad kutoka kwa baba yake amesema: ''Hakika Ali bin Husein alikuwa anapoadhini akisema: *"Hayya'ala khayril a'mali"* na hiyo ndiyo adhana ya awali.[63]

60 *Dalailus-Swiduq* Juz. 3, Uk. 100 sehemu ya 2 kutoka kitabu *Mabadiu Fiqhul-Islami* Uk. 37 cha Arafi chapa ya mwaka 1354 A.H, na kitabu *Muhalla* Juz. 3, Uk. 160.

61 *Wasailus-Shi'ah* Juz. 4, Uk. 645 hadithi 12 mlango namna ya adhana. *Jaamiu Ahadiithus-Shi'ah* na *Qamuusur-Rijaal*.

62 *Jawail Akhbar Wal-Athaar* kimetolewa kutoka kitabu *Lujnat Bahruz-Zikhaar* Juz.. 2 Uk. 191 na kitabu *Imam Swadiq Wal-Madhaib Arba'at* Juz. 284.

63 *Sunanul- Bayhaq* Juz. 1 Uk. 625 hadithi ya 1993. *Dalailus- Swiduq* Juz. 3 Uk. 100 sehemu ya pili kutoka kwa *Mabadiu Fiqhul-Islami* Uk. 37 kutoka kitabu *Muswannaf* cha Ibnu Abu Shayba na *Jawail Akhbar Wal-Athaar* Juz. 2 Uk. 192

Kwa mantiki gani amesema sentensi hii: "Na hiyo ndiyo adhana ya awali." Je! inafaa kuizingatia kauli yake? Jibu: Ndio, kwa sababu katika adhana ya Mtume (s.a.w.w) maneno hayo yalikuwapo.[64]

ii. Na Halabi na Ibnu Hazm na wengineo wamesema: Kwa hakika hayo yamenakiliwa kutoka kwa Ali bin Husein (a.s).

iii. Tumepokea kutoka kwa Ali bin Husein (a.s) amesema: Hakika Mtume (s.a.w.w) alikuwa anaposikia adhana husema kama vile asemavyo Mwadhini, na anasema: *"Hayya' ala Sswalaat, Hayya'alal Falaah, Hayya'ala Khayril a'mali"* Mtume (s.a.w.w) husema: *"La Hawla wala Quwwata ila Billah"*…..hadi mwisho.[65]

iv. Imepokewa kutoka kwa Muhammad bin Ali (a.s.) kutoka kwa babu yake Ali bin Husein (a.s) amesema: Pindi yanaposomwa maneno: *"Hayya'alal Falaah"* yeye alikuwa anasema: "*Hayya'ala khayril a'mali*."[66]

**Yaliyopokewa kutoka kwa Imam Baqir (a.s.):**

i. Imam Baqir (a.s) amesema: "Na maneno haya: *"Hayya'ala khayril a'mali"* yalikuwa katika adhana, Umar bin Khattabi akaamrisha wayaaache ili kuchelea watu wasipuuze Jihad na kujidhatiti na kujali zaidi Swala."[67]

64 *Dalailus-Swiduq* Juz. 3 Uk. 100 sehemu ya pili kutoka kwa *Mabadiu Fiqhul-Islami* Uk. 37.

65 *Da'aimul-Islam* Juz. 1 Uk. 145 na *Biharul-Anwar* Juz. 84 Uk. 179.

66 *Jawahir Akhbar wal Athaar* Juz.. 2 Uk. 192 cha Sa'adi.

67 *Bahruz Zikhaar*; *Jawahri Akhbar Wal-Athaar* Juz. 2, Uk. 192. Pambizo ya hivyo viwili.

ii. Imepokewa kutoka kwa Abu Ja'far (a.s) amesema: "Maneno: *"Hayya'ala khayril a'mali"* yalikuwa ni sehemu ya maneno ya adhana zama za bwana Mtume (s.a.w.w), zama za Abu Bakr na mwanzoni mwa zama za Umar bin Khattabi, kisha Umar akaamrisha yaondolewe na kuyafuta katika adhana na iqama."

Alipoulizwa kuhusu hilo, akasema: "Iwapo watu watasikia kuwa Swala ni bora zaidi kuliko amali nyingine watazembea kuhusu Jihadi na wataiacha."**[68]**

Na tumepokea yanayofanana na hayo kutoka kwa Imam Ja'far bin Muhammad Swadiq (a.s).**[69]**

Na imebakia maneno: *''Hayya'ala khayril a'mali"* ni kauli mbiu ya Ma'alawi na Ahlul Bayt na wafuasi wao kwa karne na karne, hadi yalipoanza mapinduzi ya Husein bin Ali, mwandishi wa Fakh aliandika hivi: ''Abdullah bin Hasan Aftwas alipanda mimbari ambayo ipo sehemu ambayo kipo kichwa cha Mtume (s.a.w.w) mahala pa jeneza, mwadhini akaadhini kwa kusema: "*Hayya'ala khayril a'mali*" alisema kipengele hicho alipouangalia upanga uliokuwepo mkonono mwake, aliyekuwa gavana wa Mansur katika mji wa Madina aitwaye Amry aliisikia adhana hiyo akahisi kuwepo shari, hapo akatishika na kupiga ukulele: "Fungeni mlango na nipatieni chakula na maji"**[70]**

Tanukh akasema: ''Abu Faraj amempa habari kwamba amewasikia waadhini katika zama zake walikuwa wakisema kipengele hiki: "*Hayya'ala khayril a'mali."***[71]**

---

68 *Da'aimul-Islam* Juz. 1, Uk. 142 na *Biharul-Anwar* Juz.. 84, Uk. 156.

69 *Da'aimul-Islam* Juz. 1 Uk. 142 na *Bihar Anwar* Juz. 84, Uk. 156.

70 *Muqatilut-Twalibiina* Uk. 446.

71 *Nuswuwar Muhadharaat* Juz. 2, Uk. 133.

Halabi amesema: ''Baadhi yao wameeleza kwamba: 'Hakika katika dola la Bani Bawayh alikuwa mtu mmoja miongoni mwa Raafidhwa anapoadhini husema: *"Hayya'ala khayril a'mali"* na ilipofika zama za Suljuqiya wakawazuia waadhini kufanya hivyo, na wakaamrisha wabadilishe katika adhana ya asubuhi badala ya kipengele hicho waseme: *''Asswalatu khayru minan nawm"* mara mbili, hayo yalitokea mwaka 448 A.H.[72]

**MAONI YA WANAVYUONI KUHUSU IBARA *"HAYYA" ALA KHAYRIL A'MALI*"**

Wanavyuoni wa Kishia na Mafaqihi wao kulingana na hadithi zilizopokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) na kutoka kwa Ahlul Bayt wake wanasema: Kipengele: *"Hayya'ala khayril a'mali"* ni sehemu ya adhana na iqama, na haisihi adhana na iqama bila ya kipengele hicho.

Miongoni mwao: Sheikh Mufiid[73] na Sayyid Murtadha katika kitabu chake *Al-Intiswar* zifuatazo ni baadhi ya sentensi zake amesema: ''Miongoni mwa mambo ambayo wafuasi wa Maimamu kumi na wawili wanayo na watu wengine hawana ni pale wanapoadhini baada ya kusema: *"Hayya'alal Falaah"* husema: *"Hayya'ala khayril a'mali"* na dalili juu ya hilo ni kongamano la kundi hilo yenye kuonyesha ukweli wake.

Na Ahlu Sunna[74] wamepokea kwamba kipengele hicho ni kati ya mambo yaliyokuweko wakati wa bwana Mtume (s.a.w.w), lakini inadaiwa ibara hiyo iliondolewa na kufutwa, na mwenye kudai kuwa ibara hiyo imefutwa, hana dalili na hatoipata."[75]

72 *Nuswuwar Muhadharaat* Juz. 2, Uk. 133.

73 *Muqna'atu*, mlango wa adhana na iqaama cha Sheikh Mufiid aliyekufa mwaka 413 A.H.

74 *Al-Mudawanatul-Kubra* Juz. 1, Uk. 75 na *Bidayatul-Mujtahid* Juz. 1, Uk. 121.

75 *Al-Intiswar*, Mas'ala ya 35 cha Sayyid Murtadha akiyekufa mwaka 436 A.H. vile vile hivi sasa huitwa *Zaydiyya*.

Hayya'alla khayril A'mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:18 PM Page 33



Na miongoni mwa hao ni: Sheikh Tuusi,[76] Qadhi Abdul Aziz bin Baraaj Twarabulusi,[77] Ibnu Idrisi Hilli,[78] Allama Hilli,[79] Muhaqiq Urdubiili,[80] Sheikh Yusuf Bahran[81] na yumo kati yao Muhammad Hasan Najafi, na yafuatayo ni ibara ya maneno yake, amesema: "Na ilikuwaje adhana kwa kauli iliyo mashuhuri ambayo fat'wa yake tunayo, hata kama hakuna hadithi au riwaya iliyo mashuhuri sana inawezekana kuthibitisha hilo kwa njia ya Ijmaa pamoja na hadithi hiyo.

"Bali ipo ibara katika kitabu *Madariki* inayosema: 'Hakika Madhehebu ya Masahaba na nyendo zao sijui kama yupo yeyote aliyepinga.' Na katika kitabu *Tadhkira* na *Al-Muhkay* kutoka katika kitabu *Nihayatul-Ahkam* imenasibishwa kwa wanavyuoni wetu, na katika kitabu *Dhikra* imenasibishwa katika matendo ya Masahaba, na katika kitabu *Masaalik* ipo ibara inayosema: 'Masahaba na watu wengine hawakutofautiana katika hilo.' Vivyo hivyo sentensi hiyo ipo katika kitabu *Al-Muhka* imenakiliwa kutoka katika kitabu *Muhadhabu*, bali ni lililodhihiri wala halina shaka ni lenye kujitosheleza hilo, na limethibiti kwa Ijmaa kwamba adhana ina vipengele 18 havizidi wala kupungua, navyo ni: Takbiira mara 4, Shahada juu ya tawahiid mara 2, Shahada juu ya Mtume (s.a.w.w) mara 2, Hayya' alas-Swalat mara 2, *Hayya'alal Falah* mara 2, *Hayya'ala khayril a'mali* mara 2, Takbiira mara 2 na hatimaye Tahliil mara 2.

76 *Al-Khilaf* Juz. 1, Uk. 278 na 279 kitabu cha Swala, Mas'ala ya 19 na 20 cha Sheikh Tuusi aliyefariki mwaka 460 A.H.

77 *Al-Muhadhab* Juz.. 1, Uk. 88 mlango wa adhana na iqaama cha Ibnu Baraaj aliyefariki mwaka 381A.H.

78 *Sarail* Juz. 1, Uk. 213 kitabu cha Swala na hukmu ya adhana na iqaama, cha Ibn Idris Huly aliyefariki mwaka 598 A.H.

79 *Tadhkiratul-Fuqahai* Juz. 3, Uk. 41 Mas'ala 156 idadi ya milango ya adhana na iqaama cha Allama Huly aliyefariki mwaka 726 A.H.

80 *Majmau Faidat Wal-Burhan* Juz. 2, Uk. 170 kitabu cha Swala, namna ya adhana na iqaama cha Muhaqqiq Uldubiili aliyefariki mwaka 993 A.H.

81 *Hadaiqun-Naadhirat* Juz. 7, Uk. 262 milango ya adhana na iqaama cha Sheikh Yusuf Bahraani aliyefariki mwaka 1186 A.H.

"Kila kipengele mara mbili, bali katika kitabu *Muutabar*, *Tadhkirat* na *Al-Muhka* kutoka katika kitabu *Naswiriyaat*, *Bihar* na *Muntaha* ni kwamba kwa mujibu wa Ijmaa Tahliil ya mwisho husomwa mara mbili, bali imepokewa kutoka kwa wa mwisho mwisho kwamba: Takbiira ya mwanzo ni mara nne.

"Ama kuhusu Iqama, vipengele vyake ni kauli iliyo mashuhuri baina ya watu watukufu na mashuhuri, bali kutoka katika kitabu *Muntaha* na *Nihaya* ni kwamba kipengele hicho hunasibishwa kwa wanavyuoni wetu, wala watu hawatofautiani kabisa kutokana na yaliyopokewa kutoka kwa *Muhadhabu*, na katika kitabu *Al-Dhikra* yapo maandiko yanayosema: 'Jambo hilo limefanywa na Masahaba, na kundi katika kitabu *Masaalik*, na husomwa mara mbili kwa kila kipengele na huongezwa katika Iqama kati ya *"Hayya'ala khayril a'mali* na Takbiiira kipengele: *"Qad Qaamat Sswalat"* mara mbili, na katika Tahliili ya mwisho katika Iqama husomwa mara moja tu, kwa hivyo huwa vipengele kumi na saba."[82]

**SABABU YA KUONDOLEWA IBARA *"HAYYA'ALA KHAYRIL AMALI"* KATIKA ADHANA NA IQAAMA NA UBAINISHAJI WA SABABU YAKE:**

Hakika imebainika kwamba katika mchakato huu wa kuthibitisha ibara: *"Hayya'ala khayril a'mali"* katika adhana kuwa ilikuweko katika zama za Mtume Muhammad (s.a.w.w), na kwamba ni sehemu na kiungo cha Adhana na Iqaama, na kilipofika kipindi cha khalifa wa pili kutokana na kuchelea watu wasipuuze na kutojali Jihadi ya dini ya Mwenyezi Mungu, na watu kujali zaidi Swala, kwa hivyo akaamua kuiondoa ibara hiyo, bali aliingiwa na hofu kwamba iwapo ibara hiyo itaendelea kubakia katika adhana na iqaama ingelikuwa sababu ya watu wa kawaida kuitelekeza Jihadi endapo watu watajua kwamba Swala ni amali bora zaidi, kutokana

82 *Jawairul-Kalaam* Juz. 9, Uk. 81 na 82 milango ya adhana na iqaama cha Sheikh Muhammad Hasan Najafi aliyefariki mwaka 1266 A.H.

na yaliyomo katika Swala kama vile utulivu na amani, wangejihusisha zaidi na kutafuta thawabu zake, na kwa hivyo wangeipa kisogo Jihadi ambayo ni jambo hatari kwao na wasilolipendelea.

Kwa hivyo akaona ni vizuri kwa maoni na mtazamo wake akaondoa ibara hiyo ili kutanguliza maslahi kuliko kufuata jambo hivi hivi tu, ambalo limetoka kwa Mwenyezi Mungu mtoaji sheria.
Hakika Khalifa wa pili alisema wazi akiwa katika Mimbari (jukwaani) - kama alivyomnukuu Qawshaji ambapo ameeleza katika kitabu chake *Sharhut-Tajriid* akihitimisha mada ya Uimamu, naye ni kati ya viongozi wa wanaitikadi pamoja na wanafalsafa wa Madhehebu ya Asha’ira – Umar bin Khattabi amesema: “Mambo matatu yalikuwako wakati wa Mtume (s.a.w.w) na mimi ninayakataza, nayaharamisha na ninatoa adhabu kwa atayefanya, nayo ni Mut’atu Nisaai, Mut’atul Haji na *Hayya’ala khayril a’mali*.”

Na hakika Qawshaji ameomba samahani kutokana na hilo kwa kauli yake: “Hakika kwenda kinyume na Mujtahidi (Mtoaji fat-wa) kuchukua na kufuata Mas’ala ya mwingine katika Mas’ala ya kiijitihadi sio bidaa.”**[83]**

Na Ibnu Shadhan alipokuwa akiwahutubia Ahlu Sunna wal-jamaa alisema: Kipengele *“Hayyal’ala khayril a’mali”* kilikuweko katika adhana zama za Mtume (s.a.w.w), zama za Abu Bakr na mwanzoni mwa zama za Umar bin Khattabi, na watu walikuwa wakiadhini hivyo, lakini Umar bin Khattabi akasema: Hakika mimi ninachelea iwapo kitasomwa kipengele kinachosema: *“Hayya’ala khayril a’mali”* katika adhana, watu wataacha Jihadi, basi kuanzia hapo akaamrisha kipengele *“Hayya’ala khayril a’mali”* kiondolewe katika adhana…”**[84]**

Imepokewa kutoka kwa Akrama amesema: “Umar alitaka watu wasijali zaidi Swala na kuacha Jihadi, kwa hivyo akakiondoa kipengele hicho kati-

83 *Sharhut-Tajriid* Uk. 484 cha Qawshaji.
84 *Al-Idhaau* Uk. 201 na 202.

ka adhana."[85]

Na Sa'ad Diin Taftazani ameeleza katika mstari wa pambizo ambapo ameuandika katika kitabu *Sharh A'dhdu Ala Mukhtasari Usuul* cha Ibnu Hajib amesema: "Hakika kipengele *"Hayya'ala khayril a'mali"* kilikuweko katika adhana wakati wa Mtume (s.a.w.w), na hakika Umar ndiye aliyewazuia watu kusoma kipengele hicho kuchelea watu kuacha Jihadi na kujali zaidi Swala."[86]

Nasema: Ikiwa kipengele hicho ni sababu ya kuwafanya watu wapuuze Jihadi ingelikuwa bora zaidi kutoanzishwa na kufanywa kuwa sheria, kwa sababu kinaleta uharibifu, ufisadi na uovu wa kudumu, na kwa maana hiyo tunawaona Ahlu Sunna wal-jamaa wamekiacha kipengele hicho hadi hivi leo, hilo la kwanza.

Pili: Hakika Mtume (s.a.w.w) – yeye ndiye aliyebashiri kuporomoka utawala wa Kisra na Qaysar – ndiye aliyestahili kudiriki na kuutambua uzembe na uzorotaji huo, iwapo utatokea baada yake kama inavyodhaniwa.

Tatu: Hakika ushujaa na ujasiri wa Masahaba vitani unakadhibisha uzorotaji na uzembeaji huo unaodhaniwa, kwani wao walikuwa wakipigana kutetea dini ya Mwenyezi Mungu wakiwa pamoja na Mtume (s.a.w.w), na kipengele *"Hayya'ala khaiyri a'mali"* hakikuwazuia wao hilo, kama vile Qur'ani tukufu inavyosema kinaga ubaga.[87]

---

85 *Biharul-Anwar* Juz. 84, Uk. 130 na *I'lalus-Shara'iu* Juz. 2, Uk. 56.

86 *Dalailus-Siduq* Juz. 3, Uk. 100 sehemu ya 2 kutoka kitabu *Mabadiu Fiqhul-Islami* Uk. 38 cha Arafi na *Siiratul-Mustafa* Uk. 274 cha Sayyid Hashim Maarufu, kutoka kitabu *Raudhun-Nadhiir* Juz. 2, Uk. 42.

87 Qur'anii Sura 9 aya 111 na 112.

Hayya'alla khayril A'mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:18 PM Page 37



Na hakika Qawshaji mwanafalsafa wa Ashaira ameomba samahani kwa maneno yake aliposema: "Hakika sio bidaa kumkhalifu Mujtahidi (mfutu mas'ala ya kidini) na kwenda kwa mwingine katika masuala ya kiijitihadi."[88]

Na uombaji udhuru huo haukubaliki, tutakapochunguza kwa uangalifu na makini tunaona kwamba Mtume (s.a.w.w) hatamki kwa matamanio yake isipokuwa kwa matakwa ya Mola Manani, Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ وَمَا يَنطِقُ عَنِ ٱلۡهَوَىٰٓ ۝٣ إِنۡ هُوَ إِلَّا وَحۡيٞ يُوحَىٰ ۝٤ ﴾

**"Wala hasemi kwa tamaa (ya nafsi yake) ni ufunuo anaofunuliwa."(*Sura Najm*: 3 – 4)**

Amesema Sayyid Sharafu Diin katika kuchambua maneno hayo akasema: "Lakini kiini cha udhuru kwamba Khalifa wa pili ni kwamba aliona hakika wao watajali zaidi Swala na kupuuza na hata kuacha Jihadi, kama Khalifa wa pili alivyosema wazi wazi. Huchunguzwa kwa undani maneno ya Qawshaji pale aliposema: 'Hakika sio bidaa kumkhalifu Mujtahidi na kwenda kwa mwingine katika Mas'ala ya kiijitihadi …' Hakika uombaji samahani haukubaliki wala hauthibiti kwa sababu Mtume (s.a.w.w) ameeleza kwamba haifai kuikhalifu na kwenda kinyume na hadithi (maandiko), kwa hivyo hukumu zinazotoka kwa Mtume (s.a.w.w) zinafungamana na matendo ya watu wazima haifai kwenda nayo kinyume, kwani halali ya Muhammad ni halali mpaka Siku ya Kiyama, na vivyo hivyo haramu yake ni haramu hadi Siku ya Kiyama.

"Hali kadhalika Mas'ala ya hukumu zake sawa zile ambazo humuelekea mtu mzima moja kwa moja au zile ambazo humwelekea lakini sio moja kwa moja, na hilo wamekubaliana waislamu wote kama walivyokongamana juu ya utume wake, hakuwa anaye hubutu kusema tofauti na hivyo.

88 *Sharhut-Tajriid* Uk. 484 cha Qawshaji.

"Qur'ani tukufu inaeleza kinaga ubaga kuhusu uhakika huo; Mwenyezi Mungu anasema:

﴿ وَمَآ ءَاتَىٰكُمُ ٱلرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَىٰكُمْ عَنْهُ فَٱنتَهُوا۟ ۚ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ ۖ
إِنَّ ٱللَّهَ شَدِيدُ ٱلْعِقَابِ ﴿٧﴾ ﴾

**"Na anachokupeni Mtume basi pokeeni, na anachokukatazeni basi jiepusheni na mcheni Mwenyezi Mungu, kwa hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu." (*Sura Hashri*: 7)**

"Na anasema:

﴿ وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥٓ أَمْرًا أَن يَكُونَ لَهُمُ ٱلْخِيَرَةُ
مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَن يَعْصِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَٰلًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾ ﴾

**"Haiwi kwa mwanaume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanapokata shauri, wawe na hiyari katika shauri lao, na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake hakika amepotea upotovu ulio wazi." (*Surat Ahzab*: 36)**

"Vile vile anasema:

﴿ فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا۟
فِىٓ أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا۟ تَسْلِيمًا ﴿٦٥﴾ ﴾

**"Naapa kwa Mola, hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye hakimu (wao) katika yale waliyokhitilafiana kati yao, kisha wasione dhiki nyoyoni mwao juu ya hukumu uliyotoa na wanyenyekee kabisa." (*Sura Nisai*: 65)**

"Aidha anasema:

﴿إِنَّهُۥ لَقَوۡلُ رَسُولٖ كَرِيمٖ ۝٤٠ وَمَا هُوَ بِقَوۡلِ شَاعِرٖۚ قَلِيلٗا مَّا تُؤۡمِنُونَ ۝٤١
وَلَا بِقَوۡلِ كَاهِنٖۚ قَلِيلٗا مَّا تَذَكَّرُونَ ۝٤٢ تَنزِيلٞ مِّن رَّبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ ۝٤٣﴾

**"Kwa hakika hii ni kauli ya Mtume mwenye heshima. Wala hiyo si kauli ya mshairi, ni kidogo tu mnayoyaamini. Wala si kauli ya mchawi, ni kidogo tu mnayokumbuka. Ni uteremsho kutoka kwa Mola wa viumbe vyote." (*Surat Al-Haqa*: 40 - 43)**

"Na anasema:

وَمَا يَنطِقُ عَنِ ٱلۡهَوَىٰٓ ۝٣ إِنۡ هُوَ إِلَّا وَحۡيٞ يُوحَىٰ ۝٤ عَلَّمَهُۥ شَدِيدُ ٱلۡقُوَىٰ ۝٥

**"Wala hasemi kwa tamaa (ya nafsi yake). Hayakuwa haya ila ni Wahyi uliofunuliwa. Amemfundisha Mwenye nguvu sana." (*Sura Najm*: 3 - 5)**

Na akamsemesha Mtume (s.a.w.w) kama vile Qur'ani tukufu inavyosema:

﴿لَّا يَأۡتِيهِ ٱلۡبَٰطِلُ مِنۢ بَيۡنِ يَدَيۡهِ وَلَا مِنۡ خَلۡفِهِۦۖ تَنزِيلٞ مِّنۡ حَكِيمٍ حَمِيدٖ ۝٤٢﴾

"**Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake kimeteremshwa na Mwenye hekima, Mwenye kuhimidiwa." (*Sura Fuswilat*: 42)**

"Haipasi kwa mwenye kuamini Aya hizo au kusadikisha Utume wake (s.a.w.w) ajiweke kando na maelezo yake (ya Aya hizo) kwa kisingizio kisicho na msingi ambacho hutofautiana nazo, haipasi wawe wapotoshaji, bali wawe wafafanuaji na wachambuaji."[89]

89 *Naswu Wal-Ijtihad* hotuba ya kitabu.

Hayya'alla khayril A'mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:18 PM Page 40



## NYONGEZA KATIKA KUTILIA MKAZO MAELEZOYAHUSUYO IBARA *"HAYYA"ALA KHAYRIL A'MALI"*

Zarkushi katika kitabu chake *Bahru-Muhiit* amesema: "Na miongoni mwa hayo yapo waliyotofautiana, kama tofauti iliyopo katika Mas'ala nyingine, na alikuwa mtoto wa Umar ambaye ndiye tegemeo la watu wa Madina, anaona kipengele kinachosema: *"Hayya'ala khayril a'mali"* ni kipengele kati ya vipengele vya adhana. Na katika kitabu *Sinamu* ni haya hapa matamshi yake: Ni sahihi kwamba adhana ilianzishwa ikiwa pamoja na kipengele *"Hayya'ala khayril a'mali."*

Katika kitabu *Raudhun-Nadhir*: Hakika wanazuoni wengi na wafuasi wa madhehebu ya Malik na Madhehebu ya Hanafii wamesema: "Hakika kipengele *"Hayya'ala khayril a'mali"* ni miongoni mwa matamshi na maneno ya adhana.

Na Shaukani akinukuu kutoka katika kitabu *Ahkam* amesema: "Hakika imesihi kwa mujibu wa hadithi sahihi kwetu, kwamba kipengele *"Hayya'ala khayril a'mali"* kilikuwa zama za Mtume (s.a.w.w), wakati wa kuadhiniwa kipengele hicho kilikuwa kikitajwa, hakikuondolewa isipokuwa katika zama za Umar."**[90]**

Imebainika kutokana na yale yaliyokwishatangulia kuhusiana na mchakato huu wa kuthibtisha, ni kwamba kipengele *"Hayya'ala khayril a'mali"* kilikuwa kikisemwa na kutamkwa zama za Mtume (s.a.w.w), zama za Abu Bakr na zama za Umar bin Khattabi, hadi pale alipofanya ijitihadi ya

90 *Naylul-Awtwar* Juz. 2, Uk. 32 cha Shawkani Yamaniy Zaydiy, vivyo hivyo wasema katika adhana watu wa madhehebu ya Zaydiyya hadi hivi sasa.

kukiondoa, na ikiwa hilo limetokea kweli, sisi hatuwezi kuutambua utetezi wowote ule ambao unahalalisha juu ya kuachwa kwa kipengele hicho katika zama hizi, na kwa nini haturudi katika Sunna ya Bwana Mtume (s.a.w.w) pamoja na Ahlul Bayt wake watoharifu?!

Kwa kutumia ushahidi na nguvu ya hoja mbali mbali imebainika na kudhihirika kwamba kipengele: "*Hayya'ala khayril a'mali*" ni kipengele kati ya vipengele vya Adhana na Iqama ambacho kilikuweko toka mwanzo, na kikaendelea hivyo katika zama za Khalifa wa kwanza na kipindi fulani katika zama za Khalifa wa pili, na Khalifa wa pili ndiye aliyeamrisha kipengele hicho kiondolewe, bila hoja ya msingi na isiyokidhi haja, ambacho Bwana Mtume (s.a.w.w) alikiweka na kukithibitisha.

## OORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION:

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu

27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Amateka Na Aba'Khalifa
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Nyuma yaho naje kuyoboka
41. Amavu n'amavuko by'ubushiya
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu

Hayya'alla khayril A'mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:18 PM Page 44



58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Sadaka yenye kuendelea
86. Msahafu wa Imam Ali

87. Uislamu na dhana
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
97. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
98. Swala ya maiti na kumlilia maiti
99. Shiya na Hadithi (kinyarwanda)
100. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
101. Hadithi ya Thaqalain
102 Fatima al-Zahra
103. Tabaruku
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Mahdi katika sunna
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa

Hayya’alla khayril A’mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:18 PM Page 46



114. Iduwa ya Kumayili.
115. Maarifa ya Kiislamu.
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehmu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehmu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Idil Ghadiri
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Kwanza
131. Imam Ali binamu ya Mtume Sehemu ya Pili
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?

140. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Kwanza
141. Uislamu na Mazingatio Sehemu ya Pili
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu *Fiqhi al-Sunnah*
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 1
153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 3
155. Abu Huraira
156. Kati ya Alama kuu za dini Swala ya Jamaa.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu sehemu ya Pili
161. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
162. Falsafa ya mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Huduma ya Afya katika Uislamu
164. Hukumu za Mgonjwa

Hayya'alla khayril A'mali katika Adhana Lubumba Dr. Kanju.qxd 7/1/2011 4:18 PM Page 48



165. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein
166. Uislamu Safi
167. Majlis ya Imam Husein
168. Mshumaa
169. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
170. Uislam wa Shia
171. Amali za Makka
172. Amali za Madina
173. Uislamu na mfumo wa Jamii ya dini nyingi
174. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
175. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
176. Elimu ya Tiba za Kiislam Matibabu ya Maimamu
177. Falsafa ya Dini

# BACK COVER

Kitabu hiki kimeshughulikia tamko la Adhana ambalo limo katika Adhana ya Mashia na ambalo halimo katika Adhana ya Masunni. Tamko hilo ni: "*Hayya'alla khayril A'mali*."

Wanachouni wa Kiislamu kama kawaida ya wanadamu wamehitilafiana katika hukumu ndogo ndogo katika matendo ya ibada, lakini kama ilivyo, tofauti ndogo kati ya wanachuo kwa wafuasi inakuwa ni mlima wa tofauti na kusababisha zongo lisilo na maana. Mambo ambayo wanachuo wetu wamehitilafiana si katika asili au misingi ya dini, na isitoshe ni mambo machache sana ukilinganisha na yale tunayokubaliana nayo.

Je, maneno "*Hayya'alla khayril A'mali*." katika adhana yana asili katika Dini? Ili kulielewa vizuri suala hi ungana na jopo la wanachuoni ambao wameliletea ufafanuzi wa kina suala hili.

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**

**Alitrah Foundation**

S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: alitrah@raha.com

Tovuti: www.ibn-tv.com

Katika mtandao: www.alitrah.info